

Shairi lifuatalo, liliandikwa na Marehemu Hamidu Tambwe, miaka kadhaa iliyopita linazungumzia Mapenzi kati ya kijana ambaye bado hana uzoefu na mapenzi, lakini kwa bahati mbaya akakutana na mwanamke aliyekubuhu kwa mambo hayo na ambaye pia hakutulia, matokeo yake ni moyo kuingiwa na simanzi. Shairi la Shetani linazungumzia mapenzi kwa ujumla, na shetani kwa mantiki ya mwandishi anaweza kuwa Mwanamume au Mwanamke mwenye sifa zinazofanana na shetani aliyekusudiwa na mwandishi Hamidu Tambwe. Fundisho kubwa hapa Mapenzi lazima yachukuliwe kwa tahadhari ama sivyo moyo utajawa na simanzi.

SHETANI

1. Mwanamke maluhuni, usimfanye rafiki,
Nasema bila utani, hakika nimesadiki,
Hata akiwa jirani, abadi haaminiki,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
2. Nilimpa ta shuleni, rafiki kweli wa dhiki,
Akajalia Manani, kwa vingi tukashiriki,
Mezani madarasani, chake ni kile na hiki,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
3. Tulipoanza mapenzi, hakika tulipendana,
Yalikuwa ni mapenzi, sijawahi kukumbana,
Kumbe ni ya upuuzi, kanicheza dana dana,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
4. Kabula kunigeuka, dalili nilizona,
Moyo ulinishituka, kumuona amebana,
Kama amepumzika, kumbe anangoja bwana,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
5. Baada ya kumuona, nami chaki nikabana,
Nikamuona kijana, naye wakikonyezana,
Kisha wakenda kutana, na kuanza semezana,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
6. Walipoisha maliza, kila mtu kenda zake,
Mimi sikumuuliza, kwa kujiona ni pweke,
Moyo ukanipooza, nikamfuata kwake,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
7. Nilipofika nyumbani, alikuwa kawasili,
Akaniuliza nini, huku akiwa mkali,
Nikamwambia amani, usijipe ukatili,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
8. Baada kuona hayo, nikaondoka haraka,
Mengine sikuwa nayo, nikaamua kung' aka,
Na ikawa ndivyo sivyo, moyo ukanipinduka,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
9. Nami sikukata tama, mwingine nikampata,
Mwana alokuwa mwema, wala hanayo matata,
La! Kumbe nimeutema, ni shetani nimepata,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
10. Nikaamua kumwacha, nimtafute mwingini,
Halafu kulipokucha, nikangia mitaani,
Nilijipatia pacha, kumbe naye ni haini,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
11. Ni bure nilisumbuka, bila kibamba kupata,
Nikamuomba Rabuka, anijalie kupata,
Kumbe ninahangaika, bahati sikuipata,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
12. Niliporudi Tabora, wengine nikawaona,
Nikapata kidoshora, ambacho tukapendana,
Na kumbe yeye ni chura, si mzia ya maana,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
13. Na hapo nikasadiki, watu hawa ni shetani,
Ukiwafanya rafiki, jua umepiga chini,
Hata hawaaminiki, ukapenda weka ndani,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.
14. Kalamu chini naweka, nikae kupumzika,
Nimechoka kuandika, sitaki tena sumbuka,
Haya mambo ukitaka, shuruti kuhangaika,
Ninasema kwa yakini, usimfanye rafiki.

Hamidu R Tambwe
F.52 - Urambo
16.08.1967
23.13 hrs